PASSPORT YA MWANAFUNZI

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI**

**SHULE YA SEKONDARI MOHORO,**


S.L.P 80,

IKWIRIRI/RUFIJI.

SIMU:0768518986/0652310018

TAREHE: …………….

MAKAMU 0766954767

E-mail: *gladnessswai@gmail.com*


KUMB.NA: MOHSS/F.V/2026

MZAZI/MLEZI WA:………………………………………………………………….……….

KUTOKA SHULE YA SEKONDARI ………………………………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO MWAKA …....**

## 1.0. UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba kijana wako (mtajwa hapo juu) amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Mohoro mwaka ……. kwa mchepuo wa………..Tunampongeza sana kwa hatua hii ya mafanikio.

Shule hii ni ya Bweni (Boarding School) kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita na ina nafasi za hosteli kwa wasichana na wavulana wa madarasa ya chini (kidato cha kwanza mpaka cha nne).

Shule ya Sekondari Mohoroipo katika kijiji cha SHELA kata ya SHELA, Hlamashauri ya Mji Rufiji Mkoa wa Pwani. Mohoro ipo takribani umbali wa kilomita 207 kutoka Dar Es Salaam ukielekea barabara ya mikoa ya kusini.

Kwa wanafunzi wanaotokea mikoa ya kusini LINDI, MTWARA NA SONGEA washuke MOHORO kituo cha GOGOZEMBE na kwa wanafunzi wanaotoka mikoa mingine wafike DAR ES SALAAM-MBAGALA RANGI TATU ndipo watapata mabasi yanayokuja MOHORO moja kwa moja. Nauli ya abiria kutoka DAR ES SALAAM kuja MOHORO ni shilingi elfu kumi (14,000) tu.


Muhula wa masomo utaanza tarehe ………………….. hivyo anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe hiyo ……………….. na mwisho wa kuripoti ni tarehe ………………. ***Tafadhali asicheleweshwe ili aweze kufanya vizuri katika masomo yake.*** Ikiwa kuna sababu

yoyote isiyokwepeka itakayopelekea kuchelewa shule au ukiamua kumpeleka shule binafsi toa taarifa ya maandishi mapema kwa MKUU WA SHULE kupitia namba za simu na e mail ya hapo juu kabla ya tarehe ya kufungua shule ili kuepusha usumbufu kwako, shule au kwa serikali.

NB: Mwanao atapokelewa shuleni iwapo yeye na wewe mtayasoma maelekezo, kuyakubali na kujaza maelezo yote yaliyomo katika viambata A – F

A. Maelezo maalum ya kujiunga na shule
B. Ada na michango mbalimbali ya shule
C. Sheria, kanuni na taratibu za shule
D. Ahadi/kiapo cha mwanafunzi
E. Vitabu na vifaa vya usafi
F. Fomu ya vipimo vya afya kwa mwanafunzi (Medical Examination Form).

***Nakutakia maandalizi mema***



**GLADNESS E SWAI**

**MKUU WA SHULE**

## A.**MAELEZO MAALUM YA KUJIUNGA NA SHULE**

### I. SARE ZA SHULE:

- Shati mikono mirefu au nusu kanzu mikono mirefu - (rangi nyeupe) mbili.
  NB: Nusu kanzu ifunike makalio na ivaliwe na ushungi (hijab) nyeupe inayofunika hadi kifuani na iwe ya kupwaya (isibane mwili).
- Sketi mbili rangi ya **kijani jeshi** ndefu na ivuke magoti inch 5 au zaidi kwa kwenda chini, mshono wa rinda box.
- Sketi rangi **ya udongo (rangi kama ya sare ya jeshi la magereza)** kwa ajili ya kushindia na zitavaliwa baada ya vipindi vya darasani.
- Soksi ndefu **NYEUPE** jozi mbili au zaidi.
- Viatu **VYEUSI VYA NGOZI** viwe na visigino vifupi, vya kufunga na kamba na visivyokuwa na urembo wowote. Vibajaji na ndala HAVIRUHUSIWI.
- Raba nyeupe za michezo jozi moja
- Fulana za michezo jezi light blue( Manchester city)
- Mitandio ya kushindia ya rangi ya bluu bahari (kwa wanaotaka)
- Sweta la rangi ya kijani jeshi
- Jezi za michezo (TRACKSUIT YA BLUU BAHARI NA FULANA YA BLUU BAHARI)
- Kandambili kwa ajili ya kuogea
- Chandarua cha rangi ya nyeupe

N.B: ***Mwanafunzi awe amevaa sare wakati wa kuripoti na wakati wa kwenda nyumbani***

### II. VIFAA VYA KUJIFUNZIA

- Daftari kubwa 08 au zaidi (counter books Q3 au Q4)
- Kalamu /penseli za kutosha
- Mkebe wa vifaa vya hesabu
- Kamusi (English-English Dictionary) ya OXFORD na
- Dissecting kit kwa wanafunzi wa mchepuo wa CBG
- Scientific calculator kwa wanafunzi wa chepuo wa CBG
- Koti jeupe la maabara mikono mifupi-urefu lifike magotini kwa mkondo wa CBG
- Begi kwa ajili ya kubebea vifaa vyake vya kujifunzia.

III. **MAHITAJI YA BWENI**

- Godoro la futi 2.5 kwa 6
- Shuka tatu rangi ya bluu bahari
- Mto na foronya mbili rangi ya bluu bahari
- Sabuni, taulo, mswaki na dawa ya meno
- Nguo za ndani (chupi 12 au zaidi)
- Ndoo mbili za lita 10
- Sanduku imara la bati (tranka) moja lenye makufuri mawili
- Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kikombe, kijiko, chupa ya chai)
- Chandarua cha rangi nyeupe

IV. **MAHITAJI MENGINE**

- Picha sita (06) za passport size akiwa amevaa shati jeupe na rangi ya bluu nyuma
- Rimu mbili za karatasi A4 kwa mwaka aina ya DOPPER, DOUBLE A au MOOND
- Result slip na leaving certificate ya kidato cha nne (CSEE) halisi na nakala
- Cheti cha kuzaliwa halisi na nakala
- Picha mbili za wazazi au/na walezi watakaoruhusiwa kuja kukutembelea (passport size)
- Kadi ya bima ya afya NHIF au CHF au yoyote inayokubalika kituo cha afya
- Jembe lenye mpini, fagio laini(soft broom), panga, squeezer na fyekeo

**NB:** *Gharama ya usafiri na matibabu ni jukumu la mzazi/mlezi wa mwanafunzi*.

B. MICHANGO

| Na | Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambuisho cha shule | 5,000/= |
| **JUMLA** | | **80,000/=** |

**N.B: MALIPO YOTE YALIPWE KUPITIA BENKI YA NMB, AKAUNTI YA SHULE NAMBA 21301100053 JINA LA AKAUNTI NI: MOHORO SECONDARY SCHOOL-RECURRENT. Wakati unafanya malipo hakikisha unatumia jina kamili la mwanafunzi kama jina la MLIPAJI. Aje na risiti (pay-in-slip) ya malipo anaporipoti shuleni. Ukilipa kwa wakala wa NMB ambatanisha na risiti ya mashine ya EFD. Fedha taslimu hazipokelewi shuleni**

## C.**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku ( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**


**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**KARIBU SANA MOHORO SEKONDARI**



**GLADNESS E. SWAI**

**MKUU WA SHULE**

**D.MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

Kidato…………..…….Mchepuo………………….…mwaka…………………. Uraia ………………..…… Dini……………………Dhehebu …………………… Tarehe ya kuzaliwa……………………Mahali alipozaliwa………………………. Nambari ya cheti cha kuzaliwa……………………………………………. Kama ni mlemavu taja aina ya ulemavu………………………………………… Kijiji……………………Namba ya nyumba………………Kata……………… Tarafa ……………..Wilaya………………………Mkoa………………………….

**BABA:**

- Jina la baba………………………………………………………………..
- Je yupo hai?.............................................................................................
- Anwani yake ya sasa ni S L P ………………………………………..
- Kazi yake………………..Dini yake………………. Dhehebu……………..
- Je baba na mama wanaishi pamoja?.......................................................
- Simu ya baba…………………………… simu ya kazini………………….

**MAMA:**

- Jina la mama…………………………………………………………
- Je yupo hai?.............................................................................................
- Anwani yake ya sasa ni S L P …………………………………….
- Kazi yake……………..Dini yake…………… Dhehebu……………..
- Mwajiri wa mama……………........................................................
- Simu ya mama……………………… simu ya kazini…………………

**MLEZI**

- Jina la mlezi…………………………………………………………
- Uhusiano na mwanafunzi……………………………………………
- Anwani yake ya sasa ni S L P ……….………………………… Kazi yake….…………..Dini yake……..…. Dhehebu……………..
- Mwajiri wa mlezi………........................................................
- Simu ya Mlezi……………………… simu ya kazini………………

**NDUGU WENGINE (Pasiachwe wazi)**

| **NA** | **JINA** | **UHUSIANO** | **ANUANI** | **SIMU** |
|---|---|---|---|---|
| **1** | | | | |
| **2** | | | | |
| **3** | | | | |
| **4** | | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| BABA | MAMA | MLEZI 1 | MLEZI 2 |

**HALMASHAURI YA WILAYA RUFIJI**
**SHULE YA SEKONDARI MOHORO**

**SIMU: 0768518986**
**S.L.P 80,**

**IKWIRIRI-RUFIJI**

AHADI/ KIAPO CHA MWANAFUNZI

MIMI………………………………………………………………….Ambaye nimechaguliwa kujiunga na SHULE YA SEKONDARI MOHORO kidato cha tano mchepuo wa ………….mwaka 2026 ninaikubali na kuipokea nafasi niliyopewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo ya Taifa kwa shule ya sekondari ya Mohoro

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na yaupendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania ,familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Ninaamini vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa nikiwa hapo shuleni

i. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo niliyochaguliwa kusoma
ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa na zingine zitakazokuwa zikitolewa mara kwa mara
iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni
iv. Ikiwa nitakiuka sheria kanuni na taratibu za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa, nitakubali kurudishwa nyumbani kumwita **mzazi/mlezi** wangu ……………………………………………….. (jina la mzazi/mlezi) kwa hatua Zaidi

Saini ya mwanafunzi………………………………Tarehe……………………………

**SEHEMU YA MZAZI /MLEZI**

MIMI …………………………… ninakubali mtoto wangu ………………………………… kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari Mohoro mwaka 2026/2027 ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa. Anuani yangu ya kudumu ni ……………………………… simu…………………iwapo nitapata uhamisho na kubadili makazi nitaijulisha shule kwa maandishi.

Saini ya mzazi/mlezi…………………………………..Tarehe…………………………..

**'TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO /MAAGIZO HAYA NAKUYATEKELEZA KIKAMILIFU"**

**PRIME MONISTER'S OFFICE - REGIONAL ADMMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**RUFIJI DISTRICT COUNCIL**

**MOHORO SECONDARY SCHOOL**

**E.MEDICAL EXAMINATION FORM**

To the medical officer ……………………………………………………………………

Please examine …………..…………………………………as student in the following areas:-

• Eye sight………………………………………..…………………………………

Hearing ……………………………….……………………………………………..

• Speech ………………………………………………………………………………

• Specimen:

- Stool ………..………………………………………………… -

Urine………..……………………………………………………..

- Blood ……………………………………………………………..

• Athma/tuberculosis…………..……………………………………………………

………………………….…………………………………………………………

………………………….…………………………………………………………

• Pregnancy……………………………………………………………………………

• Hereditary diseases e.g. Diabetes, epilepsy, Sickle Cell Anaemia

……………………………………………………………..……………………Any disability to be reported…………………………………………………………

• Other diseases………………………………………………………………………..

**Medical certificate**

I have examined the above student; she/he is physically fit/unfit as a student.

Reason ……………………………………………………………………………………….

Medical officer's name …………………… Designation………….... Signature……………

Station………………………………Date …………………………Official stamp…….…….

**MAHITAJI YA VITABU**

Kila mzazi/mlezi amnunulie mwanafunzi nakala moja wapo kwa kila somo na vilevile ahakikishe amemnunulia vitabu vya Historia ya Tanzania na maadili, Academic communication na Basic Applied Mathematics (kwa wale wa CBG)

**KISWAHILI**

- Kiswahili Kidato cha Tano na Sita (Taasisi ya Elimu Tanzania)
- Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili 2 (Kilangi Enock)
- Tafsiri na Ukalimani (Mwansoko)
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI) Lazima aje nayo mwanafunzi anayesoma Kiswahili vile vile anapaswa kuja na vitabu vya RIWAYA viwili,MASHAIRI viwili na TAMTHLIYA viwili (**Chagua hapo chini kwenye orodha)**

**USHAIRI**

- Fumba linaloelea (***Nyambari C)***
- Malenga wa ziwa kuu ( ***Wallah Bin Wallah***)
- Andamo msafiri safarini ***( Mohamed K. Ghassan***)
- Wosia wa baba ***(Ahmed Mohamed Amanzy***)

**RIWAYA**

- Dunia uwanja wa fujo (***Euphrase Kezilahabi)***
- Ua la Faraja ***(W.E Mkufya***)
- Mirathi ya hatari (***C.G.Mung'ong'o***)
- Wasifu wa Siti Binti Saad ***(Shaaban Robert***)

**TAMTHILIYA**

- Mukwawa wa Uhehe ***( M.M.Mulokozi***)
- Shujaa Mirambo ( ***Emmanuel Mbogo)***
- Usaliti mjini ***(Francis Imbuga)***

**ENGLISH LANGUAGE**

- Advanced level Literature by ***N. Asheli***
- Contemporary English for advanced level by ***Francis Myawi***
- **New advanced level English by *Charles S***
- English for Advanced Secondary Schools Student's Book Form Five

| **POETRY** | **PLAY** | **NOVELS** |
|---|---|---|
| Summons poems from Tanzania ***(Richard S Mabala*** | The Government inspector (***Nikolai V Gogol)*** | Animal Farm ***( George Orwell)*** |
| Poets of Africa: Lament of the silent and other poems***( Jared Angira*)** | A Taste of Heaven **(*Farouk Topan***) | Chasing the Leopard Finding the Lion ***( Julie Wakeman)*** |
| | An Enemy Of The People | The opportunist Elite (***Nyambari C)*** |
| | | The Horizon Univeiled ( ***Fellowes Mwaisela*)** |

**LITERATURE IN ENGLISH**

Literature in English for Secondary School Student Book Form Five & Six

| POETRY | PLAY | NOVELS |
|---|---|---|
| Summons poems from Tanzania ***(Richard S Mabala*** | Betrayal in the city ***(Francis Imbuga)*** | Arrow of God ***( Chinua Achebe)*** |
| Poets of Africa 7: Boundless voices Poem From Kenya (***Arthur I Luvai)*** | I will Marry When I Want ***(Ngugi wa Thiong'o)*** | A man of the people ***( Chinua Achebe)*** |
| The Bleeding Heart and Other Poems ***( Shilia Kaaya)*** | Julius Caesar(***Willium Shakespeare)*** | A Grain of Wheat ***(Ngugi wa Thiong'o)*** |
| | Man of Kafira ***(Francis Imbuga)*** | No longer at Ease ***(Achebe)Chinua*** |
| | | Joy comes in the Morning ***( Hopolang Phororo)*** |
| | | The Lion of Yola ***( Severine Ndunguru)*** |

**GEOGRAPHY**

- Practical Geography for advanced level TIE
- Physical Geography for Advanced level TIE
- Physical Geography for Advanced level by Z Kamili

**HISTORY**

- Advanced level history for form five and six by TIE

**BIOLOGY**

- Biological Science by DJ Tylor
- Biology for secondary school student book Form Five & six by TIE

**CHEMISTRY**

- In organic chemistry by TIE
- Physical Chemistry Form five &Six by TIE
- General and Inorganic Chemistry Form Five & Six by TIE

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule - 0768518986/0652310018**
- **Makamu Mkuu wa Shule-0766954767/0692112012**
- Mwandamizi Taaluma- 0764515545
- Mwandamizi Malezi - 0758245378